

Kujiunga na Miadi yako ya KidCare Anywhere



1. Dakika 15 kabla ya miadi yako iliyoratibiwa ya matibabu ya simu, bofya kiungo kilichotumwa kwako kwa barua pepe au ujumbe wa maandishi.

- Mtu 1 pekee ndiye anayeweza kuunganisha kwenye ziara kwa kutumia kiungo hiki. Mto huduma anaweza kualika mtu mwingine mara tu ziara inapoanza.


The image shows two side-by-side screenshots of email invitations from KidCare Anywhere. Both emails have a yellow header bar with the text "KidCare Anywhere CHILDREN'S MERCY".

Screenshot 1 (Left): This is a standard invitation email. A yellow button labeled "ENTER WAITING ROOM" is circled in red. Below it, the visit details are listed: "When: Thursday, February 17, 2022", "Time: 12:25 PM CST", "Service: [redacted]", and "Patient: [redacted]". Further down, there is a link to copy the URL into a browser: "Or you can copy this link into a compatible browser <https://patient.visitnow.org/start/692ce6534f3c48946d891885b8802a2598615b4>. You could check supported browsers [here](#)". A note at the bottom states: "THIS LINK CAN ONLY BE USED BY ONE USER/PARENT and should not be shared. Patient must be present for visit.".

Screenshot 2 (Right): This is a modified version of the invitation where the URL has been partially redacted. The redacted URL is circled in red. The rest of the text is identical to the first screenshot, including the visit details, the copy-link instructions, and the note about the link being used by one user only.

2. Ikiwa hujapakua programu, bofya Download App na ufuate maagizo ya kupakua.


- Ikiwa tayari umepakua programu, bofya Open App.
- Ni bora kutumia programu, lakini unaweza kuchagua Continue katika Kivinjari na kutumia Google Chrome au Safari ikihitajika.



Kujiunga na Miadi yako ya KidCare Anywhere



Kupakua Programu




Bofya kitufe cha
Download App.






Faili itapakuliwa
kwenye kompyuta
yako. Bofya mara
mbili faili kwenye
folda ya Download.

Kokota na bwaga
programu ya Teladoc
Health Patient
kwenye folda ya
Applications.



Baada ya programu
kusakinishwa, rudi
kwenye ujumbe wa
maandishi au barua
pepe yako na ubofye
kiungo cha miadi.



Unaweza kufungua
skrini hii. Bofya
Open Teladoc
Health Patient au
Open App.

Bofya Allow ili kutoa
ruhusa kwa programu
kutumia kamera na
maikrofoni yako.


Kujiunga na Miadi yako ya KidCare Anywhere



3. Bofya Check In.




4. Pitia taarifa za mtoto wako na kisha ubofye Confirm.



5. Programu itajaribu muunganisho wako wa intaneti, maikrofoni na kamera.


Unapaswa kujiona kwenye skrini.

- Tumia menu kunjuzi kubadilisha kamera au maikrofoni yako ikihitajika.
- Bofya Proceed ukimaliza kufanya jaribio.



6. Utawekwa katika chumba cha kusubiria mtandaoni. Mto huduma atajiunga wakati wa ziara yako baada ya kukagua maelezo yako.

- USIPUNGUZE au kuondoka kwenye programu hadi baada ya ziara yako kukamilika.




MAELEZO WAKATI WA KUPIGA SIMU

- Kamera na Maikrofoni

- Hakikisha kuwa kamera na maikrofoni zimewashwa. Bofya kitufe ili kuwasha na kuzima.

- ON  

- OFF  

- Bofya kitufe cha Settings ili kubadilisha kamera au maikrofoni yako.




Kujiunga na Miadi yako ya KidCare Anywhere



- Unaweza kutuma ujumbe wa mazungumzo kwa mtoe huduma wako wakati wa ziara hiyo. Bofya kitufe cha Chat ili kufungua mazungumzo.

- Andika ujumbe wako na bofya Send.



- Kumaliza ziara, bofya kitufe cha End Call.

- Ukitata simu kabla ya kumaliza, unaweza kubofya kiungo kutoka kwenye barua pepe yako au ujumbe wa maandishi na uingie tena. Hii inafanya kazi tu ndani ya dakika 5 baada ya kumaliza ziara.




Utatuzi wa shida

- Nina matatizo ya kamera au maikrofoni.

Ikiwa unatumia programu, fuata maelekezo haya ili kufikia mipangilio ya ruhusa ya kamera.

1. Fungua System Preferences kwenye Tool Bar.



2. Bofya Security na Privacy.




3. Bofya Privacy.

4. Bofya Camera

5. Hakikisha programu unayotumia kwa ziara yako imewekwa alama (Teladoc Health Patient, Google Chrome au Safari).

6. Bofya aikoni ya kufunga. Ingiza jina lako la mtumiaji na nenosiri ikiwa inahitajika.




Kujiunga na Miadi yako ya KidCare Anywhere




Ikiwa unatumia Google Chrome au Safari, fuata maelekezo haya ili kufikia mipangilio ya ruhusa ya kamera kwenye kivinjari.

Google Chrome


1. Bofya kwenye menu ya vitone 3 iliyo upande wa kulia wa upau wa kivinjari wa Chrome.




2. Bofya Settings.



3. Bofya Privacy and security kwenye menu iliyo upande wa kushoto wa skrini.



4. Bofya mshale karibu na Site Settings.



5. Tafuta ambapo "patient.visitnow.org" imenorodheshwa na bofya mshale upande wa kulia.

- Unaweza kuona "visitnow.org" badala yake.



Kujiunga na Miadi yako ya KidCare Anywhere




6. Hakikisha kuwa Camera na Microphone zinasema Allow. Kama sio, chagua Allow kwenye menu kunjuzi.




Safari


7. Bofya aikoni iliyo juu ya skrini na herufi "AA" na ubofye "Website Settings"




8. Kwenye "Camera" and "Microphone" hakikisha "Allow" imewekwa alama.




9. Bofya "Done" kurudi kwenye ziara.



10. Bofya kitufe cha kuonyesha upya kwenye upau wa kivinjari.



- Sijaweza kupata kiungo cha ziara yangu.
- Kiungo hutumwa kwa barua pepe na simu yako mara nyingi kabla ya wakati wa ziara yako.
 - Saa 24 kabla
 - Dakika 15 kabla
- Mtu 1 pekee ndiye anayeweza kuunganisha kwenye ziara kwa kutumia kiungo hiki. Mtoa huduma anaweza kualika mtu mwingine mara tu ziara inapoanza.
- Tafuta "Visitnow" kwenye ujumbe wako wa maandishi au barua pepe
 - Hakikisha kuwa umeangalia folda zako za barua pepe Takataka au Taka



Kwa usaidizi wa kiufundi, piga simu (816) 302-7895

Ili kupanga upya miadi yako, piga simu (816) 234-3700